Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
**Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

# ELIMU *Bulletin*

JARIDA LA MTANDAONI: *Toleo Na.33* - **2024**

wizara_elimuTanzania wizara_elimuTz www.facebook/moestvt.com www.wyestu.blogspot.com www.moe.go.tz ELIMUTZ

*Elimu Ujuzi Mwelekeo Mpya*




## Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la 2023

## Sasa Rasmi



# MKENDA:

## Wasomi jadilini Historia ya nchi kwa uzalendo kuchochea maendeleo

**- KAZI IENDELEE -**





## BODI YA UHARIRI

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
***Kamishna wa Elimu***

Atupele Mwambene
***Mkurugenzi wa Sera na Mipango***

Sylvia Lupembe
***Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini***

Nelly Mtema
***Mhariri Msaidizi na Mwandishi TSN***

**Wachangiaji:**
Oliva Kato
Elizabeth Pancras
Veronica Chitunda
Nazareth Mwakabuta



**Mawasiliano**:
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
Mji wa Serikali Mtumba, Mtaa wa Afya - Dodoma
S.L.P. 10, 40479 DODOMA.
Simu: +255 26 296 3533



**Jarida hili linatolewa na**
Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia


# TAHARIRI

## Waziri Mkenda awataka wasomi kujadili historia ya nchi kwa uzalendo kuchochea maendeleo

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda amewataka Wanataaluma kutafiti na kujadili historia ya nchi kwa uwazi na uzalendo ili kuhakikisha haipotoshwi hivyo kusaidia vizazi vijavyo kuwa na taarifa sahihi ajili ya maendeleo.

Prof. Mkenda ametoa rai hiyo Visiwani Zanzibar wakati akifungua Kongamano la Kitaaluma la Maadhimisho ya Miaka 60 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar lililofanyika katika Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), ambapo amesema Wanataaluma wanapaswa kushiriki katika kuenzi Mapinduzi hayo ili kujenga jamii yenye ustawi wa kisiasa na hata kiuchumi.

"Vyuo Vikuu vina jukumu la kuchambua historia ya nchi yetu kwa uwazi na uzalendo ili kuhakikisha inatunzwa na kwamba haipotoshwi ili vizazi vinavyokuja vielewe mazuri yaliyofanyika na jinsi yalichochea uchumi ambayo ni tafsiri sahihi ya kauli mbiu ya Maadhimisho ya mwaka huu inayosema 'Tuimarishe Uchumi, Uzalendo na Amani kwa Maendeleo ya Taifa letu" alisema Prof. Mkenda.

Aidha amesisiza jamii kuzingatia na kuikumbuka kikamilifu dhana ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya Mwaka 1964, inayosisitiza binadamu wote ni sawa bila kujali hali zao.

"Zanzibar ni sehemu ya Muungano wa Tanzania, leo hii ndani ya nchi yetu tunajivunia tunaye Rais Mwanamke, tunampongeza sana Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya katika kuenzi tunu zetu na kutuletea Maendeleo kupitia sekta mbalimbali ikiwemo Uchumi, Elimu, Afya na miundombinu mingine" alibainisha Waziri Mkenda.

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) Prof. Mohamed Makame ameeleza kuwa kinaendelea kuthamini kuheshimu na kuenzi mambo yote yaliyoasisiwa kwasabsbu yameleta mafanikio makubwa ikiwepo kuwezesha kuwa na Uhuru, Umoja na mshikamano wa dhati.

Ameongeza kuwa SUZA inaendelea kuleta mageuzi katika kutoa Taaluma kuanzia ngazi ya Stashahada hadi shahada ya Uzamivu, kufanya tafiti pamoja na kutoa ushauri wa kitaaluma kwa Wadau mbalimbali.

Nae Mkuu wa Mkoa Kusini Unguja Mhe. Ayoub Mohamed amesema Kongamano hilo litasaidia kutoa uelewa kwa vijana hasa Wanafunzi na kutathimini maendeleo ya Elimu na uchumi.





Upimaji wa Ufaulu >





# Ufaulu wa upimaji wa Kitaifa Kidato cha Nne, Darasa la Nne waongezeka



Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA) limetangaza matokeo ya Mtihani Upimaji wa Kitaifa Kidato cha Pili, ambapo Jumla ya Wanafunzi 592,741 kati ya 694,769 wamefaulu sawa na asilimia 85.31. Kiwango hicho cha ufaulu kimeongezeka kwa asilimia 0.13 ikilinganishwa na asilimia 85.18 ya Wanafunzi waliofaulu Mtihani huo mwaka jana.

Akitangaza Matokeo hayo Katibu Mtendaji wa NECTA Dkt. Said Mohamed amesema Jumla ya Wanafunzi 759,799 walisajiliwa kufanya Mtihani huo, wakiwemo Wasichana 405,878 na wavulana 353,921

Kati ya Wanafunzi waliofaulu kuendelea na Kidato cha Tatu Wasichana ni 314,949 sawa na asilimia 83.66 na wavulana ni 277,792 sawa na asilimia 87.28.

Kwa upande wa matokeo ya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne amesema Jumla ya Wanafunzi 1,287,934 kati ya 1,545,330 sawa na asilimia 83.34 wamefaulu kwa kupata madaraja ya A, B, C na D.

Dkt. Mohamed amesema kumekuwa na ongezeko la ufaulu kwa asilimia 0.39 kwa Wanafunzi wanaoendelea na darasa la Tano ikilinganishwa na mwaka 2022.

Kati ya Wanafunzi hao Wasichana ni 681, 259 sawa na asilimia 84.79 na wavulana ni 606,675 sawa na asilimia 81.78.

Katibu Mtendaji huyo amebainisha Baraza la Mitihani limefuta matokeo yote ya Wanafunzi 178 waliofanya udanganyifu na Wanafunzi 3 walioandika lugha isiyo na staha katika Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne.

Pia limewafutia matokeo Wanafunzi 28 waliofanya udanganyifu na Wanafunzi 14 walioandika lugha isiyo na staha katika Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili.

Uwezeshaji Elimu nje ya Nchi >

# Serikali ipo tayari kushirikiana na taasisi yoyote katika kuhakikisha vijana na wanataaluma wanapata fursa za kusoma nje ya nchi




Haya yamesemwa na Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Omari Kipanga Jijini Dar es Salaam wakati wa ufunguzi wa mkutano wa wadau wa elimu na mabalozi wa nchi mbalimbali wa kujadili fursa za ufadhili wa masomo katika nchi zao.

Mhe. Kipanga amesema kuwa Tanzania siyo kisiwa, hivyo kuna wajibu wa kuhakikisha kuna mwingiliano wa kielimu kati ya Tanzania na nchi nyingine duniani kwa kutafuta ufadhili wa vijana kwenda kupata ujuzi na umahiri na kuruhusu watu wa nchi nyingine kuja nchini kwa ajili ya kupata elimu.

“Mkutano huu umetukutanisha wadau wa elimu kuhakikisha tunatafuta fursa za ufadhili kwa vijana na wanataaluma kwa ajili ya kwenda kuongeza ujuzi katika mbalimbali Duniani” amesisitiza Mhe. Kipanga

Naibu Waziri huyo ameongeza kuwa vijana hao watakapokwenda masomoni na kurudi nchini watalisaidia taifa kupitia ujuzi na umahiri walioupata katika maeneo ya kipaumbele kama vile Kilimo, Umeme, Maji na maeneo mengine.

Mkurugenzi wa Bright Famius Company LTD, Robert Matoke amesema taasisi yake imeandaa mkutano huo ili kuwawezesha vijana wa kitanzania kupata taarifa za fursa mbalimbali za masomo zinazotolewa na balozi zilizopo nchini kwani mara nyingi vijana wamekuwa hawapati taarifa juu ya uwepo wa fursa hizo

Ameongeza kuwa katika mkutano huo Balozi za Marekani, Uingetezaa, ufatansa na Indonesia wamepata nafasi ya kuelezea fursa za ufadhili ambazo zinaweza kuombwa na vijana wa Tanzania

Naye Koingozi wa Serikali ya Wanafunzi wa Chuo akikuu cha Dar es Salaam Ally Ahmad amesema Serikali ya Wanafunzi DARUSO itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali ili kupata fursa zaidi za ufadhili wa masomo kwa wanafunzi wanaotaka kujiendeleza zaidi mara wanapomaliza shahada zao za kwanza.



Utekelezaji Mitaala >



# Prof. Mdoe asisitiza weledi katika kusimamia utekelezaji Mitaala iliyoboreshwa

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. James Mdoe ametoa wito kwa Makatibu Tawala Wasaidizi Elimu na Maafisa Elimu wa Halmashauri Msingi kwenda kusimamia kwa weledi utekelezaji wa mitaala iliyoboreshwa ili iweze kuleta tija kwa mwanafunzi kama ilivyokusudiwa na Serikali.

Prof. Mdoe ametoa wito huo wakati akifungua Mafunzo kwa Makatibu Tawala Wasaidizi Elimu pamoja na Maafisa Elimu wa Wilaya yaliyofanyika katika ukumbi wa shule ya Msingi Bernard Bendel Kola B Morogoro.

Amesema, kama wasimamizi wa masuala ya Elimu katika ngazi ya Mkoa na Wilaya ni lazima wakasimamie vizuri utekelezaji wa mitaala hiyo iliyoboreshwa kwani tayari Wizara ya Elimu kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania imetoa mafunzo kwa Maafisa Elimu Kata na Wathibiti ubora wa elimu nchi nzima.

Amesema, Taasisi ya Elimu Tanzania itaendelea kuratibu mafunzo hayo ya utekelezaji wa mitaala iliyoboreshwa ili kuhakikisha walimu wote nchini wanapokea mafunzo hayo kupitia utaratibu wa mafunzo endelevu ya walimu kazini (MEWAKA).

Aidha, Prof. Mdoe ametoa rai kwa viongozi hao wa elimu, kufuatilia kwa undani mafunzo haya ili kufahamu namna bora ya kwenda kusimamia utekelezaji wa mtaala huo ili lengo lililokusudiwa lifikiwe bila changamoto.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) Dkt. Aneth Komba amesema mafunzo ya Mtaala ulioboreshwa kwa viongozi hao wa elimu ngazi ya mkoa na wilaya utasaidia kuongeza ufanisi na tija katika maeneo yao ya utendaji.

Ameongeza kuwa, maboresho yaliyofanyika katika mitaala hii ni pamoja na kuongeza maudhui ya kisasa, kuondoa maudhui yaliyopita na wakati na kuondoa kujirudiarudia kwa maudhui katika baadhi ya masomo, pili kupunguza wingi wa maudhui katika masomo ili kuwe na uwiano wa muda wa kujifunza, tatu maboresho katika maeneo ya ujifunzaji wa elimu ya Awali na Msingi.

Akitoa neno la shukrani kwa niaba ya Maafisa Elimu Mkoa na Wilaya Afisa Elimu Mkoa wa Songwe Mwl. Michael Ligola ameishukuru Serikali inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha nyingi katika Sekta ya Elimu.



Uboreshaji Maktaba >

# Serikali kuboresha maktaba 22 nchini

## ■ Bilioni 2 zatengwa kutekeleza kazi hii
## ■ Taasisi Binafsi yajenga Maktaba Ugweno

Serikali imetenga takriban Shilingi Bilioni 2 kwa ajili ya kuboresha Maktaba 22 ikiwa ni utekelezaji wa mpango wa kuboresha Maktaba zote nchini ili kutoa fursa kwa wanafunzi, walimu na wakazi wengine wa ndani na wanaoishi nje ya nchi kupata maarifa.

Hayo yamesemwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda wakati akizindua Maktaba iliyojengwa na Bi. Jennifer Dickson Ugweno wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro kwa ajili ya wanafunzi na wananchi wa eneo hilo.

Akizungumza katika hafla hiyo Prof. Mkenda amesisitiza kuwa wadau Binafsi wanakaribishwa kuwekeza katika kujenga Maktaba maeneo mbalimbali nchini na kuwashukuru wadau waliojitoa kushiriki kujenga Maktaba hiyo ya Ugweno.

"Nichukue fursa hii kuwataka Wazazi wengine kuiga mfano wa Wazazi wa Jennifer kuanzisha Maktaba hii. Pia ninawasihi watoto wengine kuiga mfano huu wa kurudisha kwa jamii ili Taifa liendelee kupiga hatua kupitia Vijana wetu" alibainisha Waziri Mkenda.

Nae Mwanzilishi wa Maktaba Bi. Jennifer amesema ameanzisha Maktaba hiyo ili kutimiza ndoto yake ya muda mrefu kuhakikisha upatikanaji wa huduma hiyo katika eneo alilotoka.

"Maktaba hii pia ni mchango wangu na wa wale walioniunga mkono, katika kuunga mkono juhudi za serikali zinazolenga kuboresha sekta ya elimu nchini" alisema Jennifer.

Aisha amewashukuru Wanajumuiya wa Msangeni kwa michango yao pamoja na wafadhili mbalimbali ikiwemo Bayport Tanzania, Barrick Gold Mine Tanzania, Dayosisi ya Mwanga ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT-MD).

Kwa upande wake Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Prof Bonaventure Rutinwa, amesema kuwa maktaba hiyo ni miundombinu ya kielimu inayomwezesha mtu wakiwemo watoto wadogo kupata elimu ya ziada kupitia usomaji wa vitabu.



Elimu ya Amali >



# Shule 96 kuanza kutoa elimu ya Sekondari mkondo wa Amali 2024

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Dkt. Franklin Rwezimula amesema jumla ya Shule 96 za Sekondari teule zitaanza utekelezaji wa kutoa masomo ya Amali, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mitaala mipya ya elimu iliyoboreshwa.

Dkt. Rwezimula ametoa kauli hiyo mkoani Morogoro wakati akifungua mafunzo kwa walimu kutoka shule teule 28 za serikali na 68 zisizo za serikali ambazo zitaanza kutoa elimu ya sekondari mkondo wa Amali katika awamu ya kwanza.

Dkt. Rwezimula amemshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwani maono yake yameleta msukumo mkubwa na kupelekea kuwa na Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la 2023.

Katibu Mkuu huyo amelipongeza Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) kwa kukamilisha kazi ya ukaguzi wa shule teule, Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) kwa kuongoza maboresho ya Mitaala ya Elimu pamoja na VETA kwa kazi ya kusimamia maandalizi ya utekelezaji wa Mitaala ya Elimu ya Amali.

Nae Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) Dkt. Aneth Komba amesema Elimu ya Sekondari Hatua ya Chini itaendelea kutolewa kwa muda wa miaka minne na imegawanyika katika mikondo miwili: Mkondo wa Elimu ya Jumla na Mkondo wa Elimu ya Amali.

"Mkondo wa Elimu ya Amali umegawanyika katika michepuo ya fani za Kilimo na ufugaji, Umakenika, Sanaa Bunifu, michezo, Ufugaji wa nyuki, Urembo, n.k. Pia Mwanafunzi atasoma masomo ya Hisabati, Elimu ya Biashara, Kingereza na Historia ya Tanzania na Maadili ili kupata stadi za msingi katika mawasiliano, stadi za maisha na uzalendo" alisema Dkt. Komba.

Kwa upande wake Katibu Mtendaji wa NACTEVET Dkt. Adolf Rutayuga amesema mitaala inayotolewa imetengenezwa na VETA na kuhakikiwa na NACTVET, hivyo amezishukuru Taasisi hizo kwa kushiriki kikamilifu kukamilisha kazi hizo kwa ufanisi.

Uboreshaji Miundombinu >

# Shule ya sekondari yenye miundombinu ya kisasa kuzinduliwa hivi karibuni

## ■ Ujenzi wafikia asilimia 96







Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda ameridhishwa na maendeleo ya ujenzi wa Shule ya Sekondari Dodoma City inayojengwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia maarufu kama Shule ya Mfano, Jijini. Dodoma.

Akizungumza baada ya kukagua ujenzi huo, Prof. Mkenda amesema kwa hatua iliyofikia na kwamba Wizara iko tayari kwa uzinduzi kabla yavkuikabidhi Ofisi ya Rais Tamisemi.

Mkenda amesisitiza kuwa uendeshaji wa shule hiyo uzingatie Sera na Mitaala mpya ambapo ametaka kuweka msisitizo katika masomo ya sayansi na kuzingatia uwepo wa mafunzo ya Amali.

Mkenda amepongeza Mkandarasi wa mradi huo (SUMA JKT) kwa kufanya kazi nzuri na kwa ubunifu, na hasa kutengeneza mfumo wa maji taka utakao wezesha kuzalisha gesi kwa kutoa maji kwa ajili ya unwagiliaji ambapo hatua hiyo itasaidia kupunguza gharama za uendeshaji wa Shule.

Mkurugenzi wa SUMA JKT Kanali Petro Mgata ameahidi kukamilisha shughuli zote zilizosalia ndani ya mwezi mmoja na kukabidhi Shule hiyo.

Kwa upande wake Meya wa Manispaa ya Jiji la Dodoma Prof. Davis Mwamfupe amesema uwepo wa Miundombinu ya viwango katika Shule hiyo ya Mfano ni kielelezo tosha kuonesha utashi wa serikali katika kuendelea kuimarisha miundombinu na kutoa Elimu bora kwa watoto wa Kitanzania, ili waweze kuchangia maendeleo ya Taifa lao na jamii lakini.

"Shule ni kivutio cha kujivunia hapa Dodoma na ninkielelezo dhahiri cha utashi wa Serikali ya Awamu ya Sita katika kujenga miundombinu bora ya Elimu" alibainisha Prof. Mwamfupe.

Shule hiyo ya Mfano inajengwa na serikali ambapo ikikamilika itakuwa na uwezo wa kupokea Wanafunzi 1,000 na tayari imeanza kupokea wanafunzi wa Kidato cha Tano ikiwa na miundombinu yote stahiki.

Elimu ni haki ya kila mtoto >



# Watoto wote waliotoka nje ya mfumo rasmi wa elimu kurejea masomoni - Prof Mkenda

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda ameiambia Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Elimu, Utamaduni na Michezo kuwa Serikali itaendelea kuhakikisha watoto wote waliotoka nje ya mfumo rasmi wa elimu kwa sababu zozote zile wanarudi shule ili kupata elimu na ujuzi na kutimiza ndoto zao za kuwaletea maendeleo binafsi na ya Taifa.

Prof. Mkenda ameongeza kuwa wizara kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) wanatarajia kufanya tathimini ya kwanza ya watoto waliokatisha masomo kwa sababu mbalimbali na kisha kurudi shuleni baada ya serikali kutoa waraka wa kuwarudisha ili kuona kama wana changamoto zozote na jinsi ya kuboresha mafunzo yao.



"Tumekubaliana na UNICEF tufanye programu ya kwanza kwa kushirikiana ya kutathimini wanafunzi waliorudi shuleni baada ya tangazi la serikali , tutakaa na kuongea nao kuangalia changamoto zilizopo na kuzitafutia ufumbuzi" amesema Waziri huyo

Ameongeza kuwa kuna programu mbalimbali za mafunzo kwa watoto na vijana walikatika masomo kupitia FDC, Taasisi ya Elimu ya Watu wa zima na wengine wamerifi katika mfumo rasmi.

Uendelezaji Vyuo vya Afya >

# Wizara tano kujadiliana mwarobaini upungufu wanataaluma vyuo vya afya



Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknojia, Wizara ya Fedha, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Uwekezaji wakutana pamoja kujadili namna ya kutatua changamoto ya upungufu wa Wanataaluma katika Vyuo Vikuu na Kati vinavyotoa Elimu ya Afya na Tiba nchini.

Kikao hicho kilichofanyika Jijini Dodoma kimeongozwa na Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. James Mdoe pia kimejadili changamoto ya miundombinu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika vyuo hivyo.


Katika majadiliano hayo Wizara hizo zimekubaliana kwa pamoja kufanya kazi kwa ukaribu ili kuzipatia ufumbuzi changamoto pamoja na kuboresha utoaji elimu katika vyuo hivyo

Kikao hicho pia kimehudhiriwa na wajumbe kutoka, TCU, NACTVET, Vyuo vya Elimu ya juu na kati vinavyotoa mafunzo ya afya na tiba



# Uboreshaji Elimu >

## Prof Mkenda akutana na Mkurugenzi USAID




Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Prof. Adolf Mkenda amekutana na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi Mkaazi wa Shirika la Kimataifa la Misaada la Watu wa Marekani (USAID), Bw. Craig Hart.

Kikao hicho kimelenga kujadili ushirikiano katika kuimarisha sekta ya Elimu , utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo na Mitaala Mipya pamoja na kushirikiana katika kufanya mapitio ya programu na miradi wanazotekeleza.

katika kikao hicho Waziri Prof. Mkenda ameambatana na Naibu Katibu Mkuu Sayansi Prof. James Mdoe, Naibu Katibu Mkuu Elimu Dkt. Franklin Rwezimula, Mkurugenzi wa Mipango Atupele Mwambene , Kaimu Kamishna wa Elimu na Mkurugenzi wa Elimu Msingi Abdul Maulid ,Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Sylvia Lupembe na viongozi wengine

## Kamati ya Bunge yaitaka Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima kujitangaza



Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Elimu, Utamaduni na Michezo imeitaka Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima kujitangaza kuwezesha vijana kujiunga ili kupata mafunzo mbalimbali yanayotolewa.

Akizungumza wakati wa ziara ya Kamati hiyo katika Ofisi za Taasisi hiyo Jijini Dar es Salaam Kaimu Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Musa Siima amesema Taasisi ya Watu Wazima inafanya kazi nzuri ya kutoa elimu kwa njia mbadala kwa vijana walio nje ya mfumo rasmi ambayo inawasaidia vijana kutimiza ndoto zao za elimu.

Ameongeza kuwa Taasisi hiyo ambayo ina programu mbalimbali za kutoa mafunzo nje ya mfumo usio rasmi ina wajibu wa kuhakikisha vijana wote waliotoka kwenye mfumo rasmi wa elimu wanapatiwa elimu na mafunzo ya ujuzi ili kuwawezesha kuchangia katika maendeleo ya nchi.

# Anuani za Taasisi zilizo chini ya Wizara

Katibu Mtendaji,
**Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU),**
Jengo la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
S.L.P 6562,
7 Mtaa wa Magogoni,
11479 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2113694, 2113691
Barua Pepe: es@tcu.go.tz

---

Mkurugenzi Mtendaji,
**Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB),**
HESLB House, 1 Mtaa wa Kilimo -TAZARA,
Barabara ya Mandela,
P.O. Box 76068,
15471 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 736 665 533/ 739 665 533
Baruapepe: ed@heslb.go.tz

---

Katibu mtendaji,
**Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA),**
Eneo la Viwanda Mikocheni,
Barabara ya Bagamoyo,
S.L.P 2624 au 32019,
14112 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2700493-6/9 na 22 2772423
Barua Pepe: esnecta@necta.go.tz

---

Mtendaji Mkuu,
**Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTVET),**
S.L.P 17007, DODOMA.
Simu: +255 26 2323 121 / 0733 77 77 51
Barua Pepe: info@nacte.go.tz

---

Mtendaji Mkuu,
**Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM),**
Nunge Street, Old Catholic Church Road,
S.L.P 71, BAGAMOYO, PWANI.
Simu: +255 23 244 0216
Barua Pepe: adem@adem.ac.tz

---

Mkurugenzi Mkuu,
**Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH),**
Barabara ya Ali Hassan Mwinyi,
S.L.P. 4302,
14113 Kijitonyama,
DAR ES SALAAM.
Simu: +255 (022) 2771358/ 2774023/ 2700749
Baruapepe: dg@costech.or.tz

---

Mkurugenzi Mkuu,
**Taasisi ya Elimu Tanzania (TET),**
Plot 132, Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S.L.P. 35094, DAR ES SALAAM.
Simu: +255 0735 041168
Barua Pepe: director.general@tie.go.tz

---

Mkurugenzi Mkuu,
**Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA),**
S.L.P 34578,
Mikocheni B, Bima Road,
DAR ES SALAAM.
Simu:
Barua Pepe: info@tea.or.tz
dg@tea.or.tz

---

Mkurugenzi Mkuu
**VETA Makao Makuu,**
Plot No. 18, Central Business Park (CBP)
Barabara ya VETA,
S.L.P 802,
26 DODOMA.
Simu: +255 26 2963661
Baruapepe: info@veta.go.tz

---

Mtendaji Mkuu,
**Tume ya nguvu za Atomic Tanzania (TAEC)**
S.L.P 743,
23114 Engutoto, Block J, Plot No 216,
ARUSHA
Simu: +255 272 9700054
Barua Pepe:dg@taec.go.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM),**
Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere Mlimani,
S.L.P. 35091, Mtaa wa Chuo Kikuu
16103 Dar es Salaam
Simu: +255222410700
Baruapepe: vc@udsm.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Ardhi University (ARU),**
Plot No. 3, Observation Hill Blok L,
University Road,
P.O. Box 35176, DAR ES SALAAM.
Simu: +255 738 357 310-12
Baruapepe: aru@aru.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi, Muhimbili (MUHAS),**
9 Barabara ya Umoja wa Mataifa,
Upanga Magharibi,
S.L.P. 65001,
11103 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2150302-6
Baruapepe: vc@muhas.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA),**
S.L.P 3000,
Barabara ya Edward Moringe, Mtaa wa Kilimo,
01 MOROGORO
Simu: +255 23 260511-4
Barua Pepe: sua@sua.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Mzumbe (MU),**
S.L.P 1, MOROGORO
Simu:
Barua Pepe: mu@mzumbe.ac.tz
info@mzumbe.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM),**
S.L.P 259,
Mtaa wa Benjamin Mkapa,
Jengo la Benjamin Mkapa,
41107 DODOMA.
Simu: +255 26 2310001/2/3
Barua Pepe: vc@udom.ac.tz
relations@udom.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Huria Tanzania (OUT),**
S.L.P. 23409,
14110 Open University Road,
Kinondoni Municipality,
DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2668820/ 2668992
Baruapepe: vc@out.ac.tz

---

RASI wa Chuo,
**Chuo Kikuu kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE),**
Taifa Road Next to Benjamin Willium,
S.L.P 2329,
15105 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2850975
Barua Pepe: principal@duce.ac.tz
dpacademic@duce.ac.tz

---

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Ushirika Moshi,**
06 Barabara ya Sokoine Moshi,
S.L.P 474
KILIMANJARO
Simu: +255 272 751 833
Barua Pepe: info@mocu.ac.tz

---

Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kushiriki Cha Elimu Mkwawa (MUCE),**
Mtaa wa Mkwawa Chuo,
S.L.P. 2513,
51111 IRINGA CBD.
Simu: +255 26 2702 751
Baruapepe: principal@muce.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST),**
S.L.P. 131,
Barabara ya 01 MUST,
01 MBEYA.
Simu: +255(0)25 2957542/4
Barua pepe: vc@mustnet.

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NMIST),**
Kampasi ya Tengeru, Barabara ya Nelson Mandela,
S.L.P. 447,
23301 TENGERU, ARUSHA
Simu +255 272970001
Baruapepe: vc@nm-aist.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere,**
S.L.P 976, Butiama, MARA
Simu:
Barua Pepe: info@mjnuat.ac.tz

---

Mkurugenzi
**Bodi ya Huduma za Maktaba (TLSB),**
27 Mtaa wa Bibi Titi Mohamed,
S.L.P 9283
DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2150048/9
Barua Pepe: info@tlsb.go.tz

---

Katibu Mtendaji,
**Tume ya Taifa ya UNESCO,**
7 Magogoni Street,
P. O. Box 20384,
11479 DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2126598/ 22 2134292
Baruapepe: info@natcom.go.tz

---

Mkurugenzi,
**Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW)**
23 Mtaa wa Bibi Titi Mohammed,
S.L.P. 20679,
11103 DAR ES SALAAM
Simu:
Baruapepe: info@iae.ac.tz

---

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Ufundi Arusha (ATC),**
Junction of Moshi-Arusha and Nairobi Roads,
P.O. Box 296,
23105 ARUSHA.
Simu: +255 (0) 27-297 0056
Baruapepe: rector@atc.ac.tz/pro@atc.ac.tz

---

Mkurugenzi,
**Kituo cha Maendeleo Dakawa,**
S.L.P 1733,
MOROGORO.

---

Mkuu wa Chuo,
**Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT),**
Kona ya Bibi Titi na Barabara ya Morogoro
S.L.P 2958
11104 DAR ES SALAAM
Simu:
Barua Pepe: principal@dit.ac.tz

---

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA),**
30 Barabara ya Kibada,
S.L.P 9193,
17107 Kigamboni,
DAR ES SALAAM.
Simu:
Baruapepe: rector@mnma.ac.tz